# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

**SHULE YA SEKONDARI KITUKUTU,**

S.L.P.155,
**IRAMBA- SINGIDA.**
22/11/2025

Mkuu wa shule: ***GASPER BERNARD NGAILLAH.***
**Simu: *0759455023/0714951495***
***Mawasiliano ya shule-*** 0752463910
Barua pepe;***kitukutusecondaryschool@gmail.com***

MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI……………………………………………………………

S.L.P………………………………………………………………………………………..

**YAH:** MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA, SHULE YA SEKONDARI **KITUKUTU** HALMASHAURI YA WILAYA YA **IRAMBA** MKOA WA **SINGIDA** MWAKA **2026**.

Tunayo furaha kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza (I) katika shule ya sekondari **Kitukutu** iliyopo Wilaya ya **IRAMBA** katika mkoa wa **SINGIDA** mwaka **2026; HONGERA NA KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI KITUKUTU!**

Shule ipo kilomita **67** kutoka Singida mjini.
Kama utapanda basi la moja kwa moja toka Dar es salaam, Moshi, Arusha N.K yaani mabasi yote yenye uelekeo wa kwenda Mwanza, Kahama (barabara ya kati) utashuka kituo kinachoitwa **KITUKUTU**, baada ya kushuka hapo utaulizia KITUKUTU SEKONDARI ambayo ipo maeneo hayo. Endapo ukianzia safari kutoka Singida mjini, Stendi Kuu ya mabasi hapo Singida utapanda gari aina ya COASTER za kwenda Igunga ambapo utashukia kituo kinachoitwa KITUKUTU. Endapo hakuna usafiri hapo Stand Kuu Singida uliza kituo cha mabasi **Msufini** ambacho pia kipo Singida mjini, hapo utapanda gari aina ya HIACE za kwenda Kiomboi ambapo utashukia kituo kinaitwa **KITUKUTU**.
Nauli kwa sasa ni shilingi **5,000**/= kutoka Singida mjini kama hapatakuwa na mabadiliko

Kama atapanda mabasi ya kutoka Tabora, Nzega, Kahama, au Mwanza kwenda Arusha au Dar es salaam ashukie kituo kiitwacho **KITUKUTU** ambacho kipo Kilomita 10 baada ya kupita mji wa Misigiri.

Muhula wa masomo unaanza tarehe **04/01/2026** Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni kuanzia **siku ya Jumamosi 02/01/2026 muda wa kuripoti ni mchana kuanzia saa saba kamili mchana hadi saa kumi na moja na nusu jioni,** Masomo yanaanza 04/**01/2026**

Tunasisitiza mwanafunzi awahi shule kwa muda na tarehe tajwa hapo juu ili kuepusha usumbufu usio wa lazima na kuendana na kalenda ya masomo. Kwa dharura yeyote au ufafanuzi piga simu kwa namba zilizowekwa hapo juu.

## 2. MAHITAJI MUHIMU YA KUZINGATIA

### 2.1 Sare ya shule

a) Sare za darasani

i. Sketi mbili (2) kwa wasichana ziwe ndefu mpaka kwenye kifundo cha mguu, kitambaa cha **draft rangi ya dark bluu** ziwe na marinda madogo (**Sio rinda boksi**).

ii. **S**uruali mbili (2) **dark blue** kwa wavulana ziwe na mikunjo chini (Turn up), ziwe na upana wa inchi 17 au 18, mbele iwe na rinda mbili kila upande na mifuko miwili ya “cross” na nyuma iwe na mfuko mmoja. Aidha inatakiwa iwe na “luksi” sita za kuwekea mkanda.

iii. Mashati meupe mawili ya shule au zaidi ya mikono mifupi kwa wasichana na wavulana.

iv. Wanafunzi wanaovaa hijabu (kijuba) iwe nyeupe na ndefu kufika usawa wa nyonga, na hijabu zote ziwe za kitambaa cheupe aina ya **halua** au **babi.** (sio kitambaa cha mpira au aina nyingine).

v. Pull neck (kaba shingo) nyeupe moja.

vi. Viatu vya shule vyeusi vya kamba jozi mbili vyenye kisigino kifupi.

vii. Mkanda mweusi wenye kifungio cha kawaida **kwa wavulana**

b) Sare ya kushindia (Shamba dress)

i. Sketi mbili (2) nyeusi kwa wasichana

ii. suruali mbili (2) nyeusi kwa wavulana

c) Sare za michezo

i. Bukta na T-shirt rangi ya dark bluu kwa wasichana na wavulana.

ii. Raba rangi nyeusi (jozi moja) kwa wasichana na wavulana.

d) Soksi nyeupe ndefu pair tatu kwa wasichana na nyeusi size ya kati pair tatu kwa wavulana.

e) **Ovaroli 01** ya rangi ya “dark bluu” kwa wavulana na wasichana.

f) Sweta yenye nembo ya shule inapatikana shuleni {Aje na tsh.15,000/=}

g) T-shirt mbili (2) zenye nembo ya shule za kuvaa nje ya darasa zitatolewa shuleni (aje na shilingi 30,000/=).

h) **Nguo za nyumbani haziruhusiwi** isipokuwa aje na kanga/kitenge/ 1 na taulo1 kwa wasichana na taulo 1 kwa wavulana atatumia wakati wa kuoga.

**PICHA YA SAMPULI YA KITAMBAA CHA SKETI YA SHULE (KITAMBAA CHA DRAFT DARK BLUU).**



**2.2 Mahitaji mengine muhimu kwa wanafunzi wote**

**(a) Vifaa vya darasani**

i. Madaftari makubwa 11 (counter book quire 3 na 4), madaftari ya mazoezi madogo aina ya msomi (11), Kalamu za wino, Mathematical set, Penseli, Rula, Dictionary, Aje na faili 1, Aje na vitabu kulingana na masomo yake kwa ajili ya kujifunzia

ii. Ream A4 moja ya karatasi kwa ajili ya mitihani

**(b) Vifaa vya kulalia**

i. Godoro jipya la sponji $ft\ 2\frac{1}{2}$ la inchi 4.

ii. Chandarua rangi nyeupe ya duara.

iii. Mashuka mawili (2) rangi ya **light blue kwa wavulana** na **pinki kwa wasichana**

iv. Blanketi 1

**(c) Vifaa vya chakula-** Sahani, Bakuli, Kijiko, kikombe, Galoni ya kuwekea maji ya kunywa.

**(d) Vifaa vya usafi binafsi**- Mswaki na dawa ya meno, Malapa, Sabuni za kufulia na kuogea.

Ndoo 2 (ya lita 20 na lita 10).

**(e) Aje na tracksuit** ya dark bluu kwa wavulana na maroon kwa wasichana zenye mistari ya rangi nyeupe pembeni.

**(f) Aje na sanduku la bati** ngumu saizi ya kati na kufuli kwa ajili ya kutunzia vifaa vyake kwa usalama. Pia begi dogo la mgongoni kwa ajili ya kubebea daftari.

(g) Wanafunzi wanaruhusiwa kuja na kofia (boshori) za dark blue na zitatumika wakati wa baridi na usiku **(zisiwe na maandishi yeyote)**.

**MAHITAJI YA KIKE**- nguo za ndani za kutosha na taulo za kike za kutosha hata kama mtoto hajavunja ungo).

**<u>VIFAA VYA USAFI.</u>**

Kila mwanafunzi atatakiwa kuja na Ufagio wa chelewa 1,Jembe lenye mpini, ufagio special mgumu wa brashi (hard broom) 1, Sabuni ya maji nzito lita tano.

NB; MAGODORO YANAPATIKANA JIRANI NA SHULE KWA SHILINGI ELFU HAMSINI (50,000) TU NA TRUCK SUTI ZINAUZWA JIRANI NA SHULE KWA SHILINGI ELFU ISHIRINI TU (20,000).

**ANGALIZO: KUHUSU AFYA**

**<u>MWANAFUNZI AJE NA BIMA YA AFYA</u>!** KAMA HANA BIMA YA AFYA AJE NA PESA TASLIM SHILINGI **TSH 50,400/=** kwa ajili ya kukatiwa bima kubwa ( NHIF).

Iwapo mwanafunzi ana **tatizo lolote sugu la kiafya** aje na ripoti ya daktari kutoka **hospitali ya serikali** na iwasilishwe shuleni siku ya kuripoti.

NINAWATAKIA MAANDALIZI MEMA, KARIBU SANA KITUKUTU SEKONDARI,

**<u>GASPER BERNARD NGAILLAH.</u>**
MKUU WA SHULE.
0759455023/ 0714951475.

# SHULE YA SEKONDARI KITUKUTU.

## MAKOSA YANAYOWEZA KUMFUKUZISHA MWANAFUNZI SHULE

i. **Utoro**
ii. **Wizi**
iii. **Uasherati, ushoga na ulawiti , Kuoa au kuolewa.**
iv. **kutoa mimba.**
v. **Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya .**
vi. **Uvutaji wa sigara au bangi.**
vii. **Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.**
viii. **Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi,kumpiga mwalimu au na mtu yeyote Yule.**
ix. **Kudharau Bendera ya Taifa**
x. **Kulala nje ya shule bila ruhusa ya Mkuu wa shule**
xi. **Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni**
xii. **Kugoma kwa namna yoyote au kuchochea vurugu**
xiii. **Kutoa lugha ya matusi au lugha chafu kwa mwanafunzi,walimu,walezi,na jamii kwa ujumla.**
xiv. **Kumdharau mwalimu, Kiongozi, Mfanyakazi na jamii kwa ujumla**
xv. **Kutohudhuria vipindi kwa uzembe**
xvi. **Kutofanya mitihani kwa makusudi/bila sababu ya msingi**
xvii. **Kushirki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.**
xviii. **Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k**
xix. **Kumiliki simu.**

**FOMU A:**

**OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**SHULE YA SEKONDARI KITUKUTU.**

## FOMU YA KUKUBALI NAFASI ALIYOPEWA MWANAFUNZI

A. **Habari za mwanafunzi**:

i. Jina kamili…………………………………………………………………….
ii. Tarehe ya kuzaliwa……………………..Wilaya……………………………
iii. Dini………………………Dhehebu………………………………………….

**Mahali atakapokuwa anaenda likizo;**

i. Jina…………………………Uhusianao……………..Mahali……………..
ii. Jina…………………………Uhusiano………………Mahali……………..

**Kukubali nafasi:**

Mimi……………………………………nimeona maelekezo ya kujiunga na shule ya Sekondari Kitukutu. Nakubali kutimiza masharti yote ya shule ikiwa ni pamoja na kutii sheria za shule. Nitakapokuwa shuleni, nitajitahidi kwa uwezo wangu wote kusoma kwa bidii na kuchapa kazi za mikono kwa bidi, kutunza mazingira, kushiriki kikamilifu ratiba yote ya shule ili kutimiza lengo la kupata elimu katika ujumla wake NA NINAAHIDI KUWA MWANAFUNZI MWEMA, MTIIFU MWENYE NIDHAMU YA HALI YA JUU.

**Saini………………………..** **Tarehe…………………………………**

B. **Habari za Mzazi/Mlezi**

i. Jina kamili……………………………………………………………
ii. Yeye ni mzazi au mlezi………………………………………………
iii. Uhusiano uliopo na mwanafunzi……………………………………….
iv. Kazi yake……………………………………………………………
v. Anwani ya kazini……………………………………………………
vi. Namba ya simu……………………………………………………….
vii. Anwani ya nyumbani…………………………………………………………
viii. Uthibitisho wa Mzazi/Mlezi:
Nimehakikisha maelekezo na maagizo yameeleweka na mtoto wnagu atafuata sheria na taratibu zote za shule ya sekondari Tumaini.

**Jina…**…………………………………..**Saini……………………Tarehe**………………

FORM B:

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

PART A:

**TO**: The Medical Officer
_______________________
_______________________
_______________________

FROM: The Headmaster
Kitukutu Secondary School
P.O.BOX 155
IRAMBA-SINGIDA

NAME OF THE STUDENT_____________________________________________________

Please examine the above named Student as to her/his fitness for joining our Secondary School 2026

Signature _________________________

PART B: MEDICAL CERTIFICATE
(To be completed by Medical Officer)

I have examined the above named person and discovered that he/she is ______________________________________________________________________________
______________________________________________________________________________
______________________________________________________________________________
______________________________________________________________________________
______________________________________________________________________________

Date______________________ Signature ________________________
Station____________________ Designation ________________________

GASPER BERNARD NGAILLAH
MKUU WA SHULE
0759455023/ 0714951475

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI KITUKUTU
S.L.P 155 KIOMBOI IRAMBA